KWA JINA LA ALLAAH, MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 12, Issue 3
14th SHA'BAAN 1432
15th July, 2011

YALIYOMO

HUKMU, ADABU NA SUNNAH ZA SAUMU [Prt.1] 1 - 4

HUKMU, ADABU NA SUNNAH ZA SAUMU [Prt I]

Na: Sheikh Muhammad Saalih Al-Munajjid

Kila sifa njema ni zenye kumstahiki Allaah, twamsifu Yeye na tunamuomba Yeye msaada na msamaha. Tunajilinda kwa Allaah na uovu wa nafsi zetu na matendo yetu maovu. Yoyote ambae aloongozwa na Allaah, basi hapana awezae kumpotoa, na yoyote Atakaemuacha kupotoka, basi hapana awezae kumuongoa. Nashuhudia yakwamba hapana mola anaestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah Peke yake, hana mshirika na nashuhudia yakwamba Muhammad ni Mtumwa wake na Mtume.

Allaah (سبحانه وتعالى) amewabariki waja Wake na majira fulani ya kheri, ambayo ndani yake *hasanaat* (thawabu) huzidishwa, *sayyi'aat* (madhambi) husamehewa, daraja za watu huinuliwa, nyoyo za waumini huelekea kwa Bwana wao, wenye kujitakasa nafsi zao hupata kufuzu na wenye kujifisidi nafsi zao hushindwa na kuharibikiwa. Allaah aliwaumba waja Wake wamuabudu Yeye kama alivyosema (tafsiri ya maana): **"Sikuwaumba majini na watu ila wapate kuniabudu."** [adh-Dhaariyaat 51:56].

Miongoni mwa matendo ya Ibada ni kufunga saumu, ambayo Allaah aliyoifaradhisha juu ya waja Wake, kama alivyosema (tafsiri ya maana): **"... Mmelazimishwa kufunga saumu kama walivyolazimishwa waliokuwa kabla yenu ili mpate kumcha Mungu."** [al-Baqarah 2:183]. Allaah amewahimiza waja Wake wafunge (tafsiri ya maana): **"Na (huku) kufunga ni bora kwenu. Ikiwa mnajua."** [al-Baqarah 2:184]. Amewaongoza wapate kumshukuru Yeye kwa kuwafaradhishiya saumu juu yao (tafsiri ya maana): **"Na pia (anakutakieni) kumtukuza Allaah kwa kuwa Amekuongozeni, ili mpate kushukuru."** [al-Baqarah 2:185].

Ameifanya saumu kuwa ni yenye kupendekeza kwao, na Akawafanyia kuwa ni rahisi ili watu wasione kuwa ni jambo gumu kuwachana na tabia zao na mazoweya yao. Amesema Allaah (tafsiri ya maana): **"Ni siku chache tu (kufunga huko)."** [al-Baqarah 2:184]

Ana Rehma juu yao na Anawaepusha na zuito na madhara, kama alivyosema (tafsiri ya maana): **"Na atakayekuwa mgonjwa katika nyinyi au katika safari (akafunga katika baadhi ya siku), basi (atimize) hisabu katika siku nye gine."** [al-Baqarah 2:184]

Basi huwa si jambo la kushangaza, yakwamba katika mwezi huu nyoyo za waumini huelekea kwa Mola wao Aliye na Rehma zaidi, wakimcha Mola wao aliye juu yao, wakitarajia kupata Malipo kutoka Kwake na ushindi mkubwa (Pepo). Kwa vile daraja ya kitendo hiki cha 'Ibada ni ya juu sana, basi hapana budi kuzisoma *ahkaam* (hukmu) zinazohusiana na mwezi wa kufunga saumu ili Muislamu apate kujua yaliyo ya wajibu, kwa min-ajil ya kuyatekelezaq, yaliyo haraam, ili apate kujiepusha nayo, na yaliyoruhusiwa, ili ajipinde nafsi yake kwa kujikataza na mambo hayo.

1. **SIYAAM:** Katika lugha ya kiarabu maana yake ni kujizuiya; katika Uislamu maana yake ni kujizuiya na vitu au mambo yenye kuharibu saumu, kuanzia alfajiri mpaka kutwa kwa jua, baada ya kutia Niya ya kufunga wakati wa usiku wake uliotangulia.

2. Umma umekubaliana yakwamba kufunga mwezi wa Ramadhân ni wajib, ushahidi unapatikana katika Qur'an na Sunnah. Amesema Allaah (سبحانه وتعالى) (tafsiri ya maana): **"Enyi mlioamini! Mmelazimishwa kufunga (Saumu) kama walivyolazimishwa waliokuwa kabla yenu ili mmpate kumcha Mungu."** [al-Baqarah 2:183].

Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Uislamu umejengwa juu ya (misingi) mitano ...."*

HUKMU, ADABU NA SUNNAH ZA SAUM[Prt.1]

miongoni mwayo alitaja kufunga katika mwezi wa Ramadhân. [Imepokewa na al-Bukhaari, al-Fat-h 1/49]. Yoyote atakaeharibu saumu yake katika mwezi huo wa Ramadhân pasi na sababu ya kisheriya atakuwa amefanya hatia ya madhambi makubwa. Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipokuwa akiwaeleza kuhusu ndoto aliyoiota: "... *mpaka nilipofika kwenye mlima, katika mahali ambapo niliposikiya mayowe makubwa. Nikauliza, 'Ni kelele za nini hizo?' Wakanijibu, 'hizo ni kelele za watu wa motoni'. Kisha nikachukuliwa [mahali pengine] na nikawaona watu wakining'inizwa kwa ukano wa visigino vyao (mivungu ya visigino au magoti), na ncha za midomo yao imeraruliwa na inatona madamu , nikauliza, 'Na hawa ni kina nani?' Wakanijibu, 'Hawa ni wale watu waliokuwa wakivunja saumu zao kabla ya wakati wa kufanya hivyo kufika,'* yaani kabla ya wakati wa kufuturu. [Swaheeh at-Targheeb, 1/420].

Amesema al-Haafidh adh-Dhahabi (رحمه الله): "Miongoni mwa Waumini imethubutu kwao yakwamba yoyote asiyefunga mwezi wa Ramadhân pasi na sababu ya kisheriya ni muovu hata kuliko mzinifu au mlevi; huwa na shaka haswa iwapo huyo kweli ni Muislamu au laa, na wao humzingatia kuwa ni mwenye ku'asi na mpotofu." Amesema Sheikh ul-Islaam Ibn Taymiyyah (رحمه الله): "Iwapo mtu hatofunga mwezi wa Ramadhân akijua yakwamba ni *Haraam*, lakini yeye akalifanya kuwa ni Halaal katika nafsi yake kufanya hivyo, basi Muuwe mtu huyo, na lau atalifanya hilo kwa sababu yeye ni mtu muovu (lakini anaamini yakwamba jambo hilo ni haraam), basi

(Endelea kwenye Ukurasa wa 2)

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)

muadhibuni kwa kutofunga." [Majmoo' al -Fataawa, 25/265].

3. **FADHILA ZA KUFUNGA:** Fadhila za kufunga ni kubwa mno, na mojawapo la yaliyopokewa kwenye swaheeh hadeeth ni kwamba Allaah Amejichagulia Yeye Mwenyewe Saumu, na Yeye Atalilipia hilo na kuzidisha thawabu zake pasi na kipimo, kama alivyosema (katika hadeeth al-Qudsi): "Isipokuwa kwa Saumu ambayo ni kwa ajili Yangu Mimi, na Mimi Ndiye nitakayemlipa kwa saumu hiyo." [al-Bukhaari, al-Fat-h No. 1904, Swaheeh at-Targheeb 1/407]. Saumu haina kitu kilicho sawa nayo, [an-Nasaa'ee 4/165, Swaheeh at-Targheeb 1/413]. Na Du'aa ya aliyefunga haitokataliwa [Imepokewa na al-Baihaqee 3/345, as-Silsilatu as-Swahiha 1797]. Mwenye kufunga ana nyakati mbili za furaha: moja ni ya pale anapofungua saumu yake na nyengine ni atakapoonana na Mola wake na kuifurahikiya saumu yake [Imepokewa na Muslim 2/807]. Saumu itamshufaiya mtu katika siku ya Malipo, na itasema, 'Ewe Mola, mimi nilimuepusha na chakula chake na matamaniwa yake ya kimwili katika wakati wa mchana, basi nakuomba uniruhusu nimshufaiye.' [Imepokewa na Ahmad 2/174, al-Haithamee akaiorodhesha isnaad yake kama Hasan katika Majma' 3/181. Angalia pia katika Swaheeh at-Targheeb 1/411]. Harufu inayotoka kwenye kinywa cha aliyefunga ni bora kwa Allaah kuliko harufu ya misk [Muslim 2/807]. Saumu ni Kinga na Ngome iliyo madhubuti inayomlinda mtu na Moto. [Imepokewa na Ahmad 2/402, Swaheeh at-Targheeb 1/411, Swaheeh al-Jaami' 3880]. Yoyote mwenye kufunga siku moja kwa ajili ya Allaah, Allaah atamuepusha uso wake kwa umbali wa miyaka sabiini kutoka kwenye moto." [Imepokewa na Muslim 2/808]. Yoyote mwenye kufunga siku moja akitarajia radhi za Allaah, iwapo hiyo ndiyo itakayokuwa ni siku ya mwisho wa maisha yake, ataingia Peponi [Imepokewa na Ahmad 5/391, Swaheeh at-Targheeb 1/412]. Peponi kuna mlango uitwao ar-Rayyaan, ambao wale wenye kufunga watauingia mlango huo, na hapana atakaeuingia mlango huo isipokuwa wao, watakapouingia mlango huo, utafungwa, na hapana yoyote atakaeuingia." [al-Bukhaari, Fat-h No. 1797]. Ramadhân ni Nguzo ya Uislamu; Qur'an iliteremshwa katika mwezi huu, na ndani yake kuna usiku ulio bora kuliko miezi elfu moja. "Inapoanza Ramadhân, milango ya Peponi hufunguliwa na milango ya Motoni hufungwa, na Mashetwani hufungwa kwa silisili. [al-Bukhaari, Fat-h No. 3277]. Kufunga katika mwezi wa Ramadhân ni sawa na kufungwa kwa miezi kumi. [Angalia katika Musnad ya Imaam-Ahmad 5/280; Swaheeh at-Targheeb 1/421].

Yoyote mwenye kufunga mwezi wa Ramadhân kwa Imaan na kuwa na matarajio ya Malipo, atasamehewa madhambi yake yote yaliyopita." [Imepokewa na al-Bukhaari, al-Fat-h No. 37]. Katika wakati wa kufungua kila Saumu, Allaah huchagua watu wa kuwawacha huru na moto. [Imepokewa na Ahmad 5/256, Swaheeh at-Targheeb 1/419].

FAIDA ZA KUFUNGA: Kuna hikma nyingi na faida nyingi katika kufunga, zenye kuhusiana na Taqwaa iliyotajwa na Allaah katika aya (tafsiri ya maana): **"... Ili mpate kumcha Mungu."** [al-Baqarah 2:183]. Tafsiri yake ni kwamba ikiwa mtu atajiepusha na mambo ya Halaal kwa kutarajia malipo kutoka kwake na kutokana na kuogopa adhabu Yake, itakuwa ni rahisi kwake kujiepusha na kufanya mambo ya Haraam. Ikiwa tumbo la mtu lina njaa, hilo litamuepusha viungo vyake vyote vyengine na kuwa na njaa au matamanio. Lakini iwapo tumbo lake litakuwa limetosheka, ulimi wake, jicho lake, mkono wake na sehemu zake za siri zitaanza kusikiya njaa. Kufunga huongoza katika kumshinda Shetwani, humiliki matamanio na kulinda sehemu nyengine za kiwiliwili. Pindi mwenye kufunga anaposikiya maumivu ya njaa, hupata kutambua jinsi masikini anavyosikiya, kwahivyo anakuwa na huruma juu yao na huwapa kitu kitakachowaondolea njaa zao. Kusikiya kuwahusu wao si sawa na kujihusisha nao kwa njaa, kama ambavyo mwenye kupeleka chombo asivyofahamu uzito wa kutembea mpaka ashuke kwenye kipando chake na aanze kutembea. Saumu hufunza nguvu za kujiepusha na matamanio na hujiepusha na madhambi, humsaidia mtu ashinde tabia na maumbile yake mwenyewe na kujiachisha na tabia alizozoeya, vilevile humzoezesha mtu kujipanga vilivyo na kufanya mambo yake kulingana na wakati upasao, suala litakalo ondoa matatizo waliyo nayo watu wengi la kukosa mipango ya kisawasawa, lau kama wangelitanabahi. Kufunga pia ni jambo lenye kuashiriya umoja wa Waislamu, kama ambavyo Umma hufunga na kufungua kwa pamoja. Kufunga pia huleta wakati muafaka kwa wale wenye kuwalingania wenzao kwa Allaah. Katika mwezi huu, watu wengi huja kwenye misikiti kwa mara yao ya kwanza na ambao hawajawahi kuja kwenye misikiti kwa muda mrefu, na nyoyo zao zikiwa wazi, kwahivyo ni lazima tuitumie fursa hii kwa kulingania kwa njia iliyo bora, kufunza mafunzo yanayostahiki na kutamka maneno yenye faida, katika haliya kushirikiyana kwa wema na matendo mazuri. Mlinganizi na asijishughulishe na wengine mpaka akajisahau nafsi yake akawa kama utambi wenye kuwaangazia wengine haliyakuwa wenyewe unateketea. Baadhi ya mambo ni wajibu (*waajib*) na mengine ni yenye kupendekezwa (*mustahabb*). Ni lazima tuhakikishe yakwamba tunakula na kunywa kitu katika wakati wa suhoor, na kwamba tunaichelewesha mpaka muda mchache tu kabla ya adhaan ya alfajiri. Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Kuleni Suhoor, kwani katika suhoor kuna Baraka."* [Imepokewa na al-Bukhaari, Fat-h 4/139]. "*Suhoor ni chakula kilichobarikiwa, na kuna uhusiano na chakula hicho katika kujitafautisha na watu walioteremshiwa Kitabu." "Tende ni chakula kizuri kilioje cha Mu'min."* [Imepokewa na Abu Daawud No. 2345, Swaheeh at-Targheeb 1/448]. Kutochelewesha Iftaar kwa sababu Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "*Watu wataendelea kuwa katika kheri nyingi maadamu* hawatochelewesha iftaar." [Imepokewa na al-Bukhaari, Fat-t 4/198]. Mtu kufungua Saumu yake kulingana na ilivyoelezwa kwenye hadeeth iliyopokewa na Anas (رضي الله عنه): "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akifungua saumu yake na tende zilizoanza kuiva (*rutwabaat*), ikiwa hakupata tende ambazo ni *rutwab*, alikuwa akifungua na zilizoiva (*tamr*), na ikiwa hakupata tende zilizoiva alikuwa akifungua na matama ya maji [Imepokewa na at-Tirmidhee 3/79, na wengineo. Amesema ni ghareeb hasan hadeeth.

(Endelea Kwenye Ukurasa wa 3)

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

Imeorodheshwa katika swaheeh hadeeth katika al-Irwaa' No. 922]. Baada ya Iftaar, kusoma maneno yapatikanayo kwenye hadeeth iliyopokewa na Ibn 'Umar (رضي الله عنه): "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa pindi anapofungua saumu yake akisema, *'Dhahaba adh-Dhama' wab'tallatil 'Urooq, wathabat al-ajru Insha-Allaah.*" *"Kiu imeondoka, na koo zimeroama, na ujira umethubutu apendapo Allâh."* [Imepokewa na Abu Dawud 2/765; isnaad yake imeorodheshwa kuwa hasan na ad-Daaraqutnee' 2/185].

Kujiepusha na madhambi, kwa sababu Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "*Atakapokuwa amefunga mmoja wenu, na ajiepushe na madhambi ...*" [Imepokewa na al-Bukhaari, al-Fat-h No. 1904]. Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "*Yoyote ambaye hatojiepusha na kutamka maneno mabaya na kutenda kulingana na mambo hayo, Allaah hana haja na kuwacha chakula chake na kinywaji chake.*" [al-Bukhaari, al-Fat-h No. 1903]. Mwenye kufunga na ajiepushe na kila aina ya vitendo vya haraam, kama vile kusengenya, maneno machafu, na kusema urongo, au huwenda malipo yake yote yakapotea. Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "*Huwenda mfungaji asipate chochote kutokana na Saumu yake isipokuwa njaa tupu.*" [Imepokewa na Ibn Maajah 1/539, Swaheeh at-Targheeb, 1/453]. Miongoni mwa mambo yenye kuharibu *hasanaat* za (mema ya) mtu na kumletea *sayyi'aat* (mambo mabaya) ni mtu kujishughulisha na mijadala ya mabishano, maonyesho ya mivutano ya kijamii, ma-Sinema na mashindano ya michezo, mikutano ya maskani, matembezi kwenye mabarabara na marafiki wabaya na wenye kupoteza nyakati, kuzurura na magari pasi na haja yoyote, kukusanyika kwenye mabarabara na vichochoro, ili miezi ya Tahajjud, Dhikr na 'Ibaada kwa watu wengi ukawa ni mwezi wa kulala katika wakati wa mchana ili mtu asipate kusikiya njaa, na kwahiyo ikawa wanakosa swala zao na fursa ya kuziswali kwa Jamaa', kisha wakatumia wakati wao wa usiku kujistarehesha na kujifurahisha nafsi zao. Baadhi ya watu pia huukaribisha mwezi kwa mambo ya maudhi, wakifikiriya tu kuhusu mambo ya starehe watakayokosa kuyafanya. Katika mwezi wa Ramadhân, baadhi ya watu husafiri na kwenda kwenye miji ya kikafiri kwa kusherehekea Siku-Kuu! Hata Misikiti pia haikuwachwa mbali na uovu huwo, kwani hujitokeza wanawake waliojipamba kwa manukato na vipodozi, na hata Nyumba Tukufu ya Allaah haikuepukika na uchafu huu. Baadhi ya watu huufanya mwezi huu kuwa ni msimu wa kuomba, hata kama wao hawahusiki miongoni mwa wanaohitaji. Baadhi yao hujitumbuiza nafsi zao kwa *fataki* (fire-works) na mfano wake, na baadhi yao hupoteza wakati wao kwa kutembea kwenye masoko au madukani, au kushona na kuandama mitindo mipya. Baadhi yao huweka bidhaa mpya na mitindo mipya kwenye maduka yao zifikapo siku kumi za mwisho za mwezi huu, kwa ajili ya kuwaweka watu mbali na kujipatia malipo mema na hasanaat. Kutojiruhusu na kuchokozwa, kwa sababu Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "*Ikiwa mtu atataka kupigana nae au atamtukana, na aseme, 'mimi nimefunga, mimi nimefunga.'*" [Imepokewa na al-Bukhaari na wengineo, al-Fat-h No. 1894]. Sababu moja ya jambo hili ni kujikumbusha nafsi yake, na sababu nyengine ni kumkumbusha adui wake. Lakini yoyote mwenye kuangalia adabu za wengi katika wanaofunga wataona kitu tafauti kabisa. Ni muhimu kwa mtu kujimiliki nafsi yake na kuwa na utulivu, lakini sisi twaona tafauti kwa madereva wenda-wazimu wanaozidisha kasi zao pindi wasikiapo miadhini wa Magharibi. (*) Kutokula kupita kiyasi, kwa sababu Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "*Mwana-adamu hajazi chombo kiovu kama tumbo lake.*" [Imepokewa na at-Tirmidhee No. 2380, amesema kuwa hadeeth hii ni Hasan-Swaheeh]. Mtu mwenye busara hutaka kula ili apate kuishi, sio kuishi kwa ajili ya kula. Sampuli bora ya chakula ni ile inayotumika, sio inayoandaliwa. Lakini watu hushughulika na kutengeza kila aina ya vyakula (wakati wa Ramadhân) na kutengeza maandalizi ya vyakula kama mapambo ya sanaa, ili wake majumbani na wafanyi-kazi watumie wakati wao wote katika kutayarisha chakula, na jambo hili huwaweka wao mbali na kufanya 'Ibaada, na watu hutumia sana kwa chakula katika mwezi wa Ramadhân kuliko wafanyavyo kwenye masiku yao ya kawaida. Kwahiyo mwezi unakuwa ni mwezi wa kuvimbiwa, kunenepa na maradhi ya matumbo, ambapo watu hula kama walafi na hunywa kama Ngamia wenye kiu, na wanapoinuka kuswali Taraweeh, huwa hawajiwezi kabisa na baadhi yao huondoka baada ya kuswali rakaa' mbili.

(*) Kuwa mkarimu katika ushirika wa 'Ilmu, kutoa pesa, mtu kutumia nafasi ya uwezo wake au nguvu zake katika kuwasaidia wenzake, na kuwa na tabia njema. Al-Bukhaari na Muslim wamepokea yakwamba Ibn 'Abbaas (رضي الله عنه) amesema: "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa ni Mkarimu sana miongoni mwa watu (katika kufanya wema), na alikuwa ni Mkarimu sana kuliko mtu yoyote katika mwezi wa Ramadhân alipoonana na Jibreel, na alikuwa akionana nae kila usiku wa Ramadhân na alikuwa akimfundisha Qur'an. Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa Mkarimu sana katika kufanya wema kuliko upepo unaovuma." [Imepokewa na al-Bukhaari, al-Fat-h No. 6]. Watu wawezaje kubadilisha Ukarimu mahala pa Ubakhili na Kutenda mahala pa Uvivu, kiyasi cha kwamba hawafanyi kazi zao kisawasawa na wakawa hawaheshimiani kisawasawa, na hutumia kufunga ikawa ni sababu ya yote hayo. Kuchanganya Saumu na kuwalisha masikini ni mojawapo ya sababu za kuifikilia Pepo, kama alivyosema Mtume (صلى الله عليه وسلم): "*Peponi kuna vyumba ambavyo nje yake huonekana kutoka ndani mwake na ndani mwake huonekana kutoka nje yake. Allaah Amewaandalia (vyumba hivyo) wale wenye kuwalisha masikini, wenye upole katika mazungumzo yao, wenye mazoweya ya kufunga na wenye kuswali katika nyakati za usiku wakati ambapo watu huwa wamelala.*" [Imepokewa na Ahmad 5/343, Ibn Khuzaymah No. 2137. al-albaani amesema katika nukta zake za chini: Isnaad yake ni hasan kutokana na riwaya nyengine zenye kuthibitisha]. Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): "*Yoyote mwenye kumpa chakula aliyefunga ambacho atakachofungulia saumu yake, atalipwa thawabu sawa na zake (huyo aliyefunga), pasi na kupunguzwa hata chembe kutokana na thawabu za aliyefunga.*" [Imepokewa na at-Tirmidhee 3/171, Swaheeh at-Targheeb 1/451]. Sheikh ul-Islaam Ibn Taymiyyah (رحمه الله): amesema: "Maana yake ni kwamba na amlishe mpaka ashibe." [Al- Ikhtiyaaraat al-Fiqhiyyah, Uk. 109].

(Endelea Kwenye Ukurasa wa 4)

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 3)

Idadi ya ma-Salaf (رضي الله عنهم) wamehitari masikini kuliko nafsi zao wanapowalisha katika wakati wa Iftaar. Miongoni mwao ni 'Abdullaah Ibn 'Umar Maalik ibn Deenaar, Ahmad ibn Hanbal na wengineo. 'Abd-Allaah ibn 'Umar alikuwa hafungui Saumu yake mpaka wawepo mayatima na masikini pamoja na yeye.

KUFANYWEJE KATIKA MWEZI HUU MTUKUFU?

(*) Kujitayarisha mtu na mazingira yake kwa ajili ya 'Ibaada, kuharakisha kutubia na kuregea kwa Allaah, kufurahi pindi mwezi unapoanza, kufunga kisawasawa, kuwa na kiunzi imara cha fahamu nzuri na kumcha Allaah unaposwali Taraweeh, kutojisikiya mchovu zifikapo siku kumi za kati na kati za mwezi, kuitafuta Laylatul Qadr, kuisoma Qur'an nzima mara kwa mara, kujaribu kuliya na kufahamu unachokisoma. 'Umra katika wakati wa Ramadhân ni sawa na Hajj, na kutoa swadaka katika nyakati hizi njema huzidishwa, na 'I'tikaaf (kubakia msikitini kwa ajili ya kufanya 'Ibaada) imethubutu (kama sehemu ya Sunnah).

(*) Hapana makosa kupongezana mwanzoni mwa mwezi. Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akiwaambia Maswahaba zake kuhusu khabari njema za kuanza kwa Ramadhân, na kuwahimiza wajitahidi kufanya mambo mazuri kwa wingi uingiapo mwezi. Amesema Abu Hurairah (رضي الله عنه): "Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): 'Imewajilia nyinyi Ramadhân, mwezi uliobarikiwa. Allaah Amewafaradhishia juu yenu kufunga (mwezi huu). Ndani yake (mwezi huo), milango ya Peponi hufunguliwa, na milango ya Motoni hufungwa, na mashetwani hufungwa kwa minyororo. Ndani yake kuna usiku ulio bora kuliko miezi Elfu moja, na yoyote mwenye kunyimwa katika kheri zake, basi amenyimwa kheri nyingi.'" [Imepokewa na an-Nisaa'ee, 4/129; Swaheeh at-Targheeb, 1/490].

BAADHI YA AHKAAM ZA SAUMU

6. Kuna sampuli ya Saumu ambazo ni lazima zitekelezwe kwa masiku mfululizo, kama kufunga mwezi mzima wa Ramadhân, au kufunga kama kafara ya kuuwa mtu kwa bahati mbaya, mtu kumuacha mkewe kwa Dhihaar [Talaka ya ki-Jahili ambayo hutokea pale mtu anapomwambia mkewe, "Wewe kwangu mimi ni kama mgongo wa Mamangu."] au kuingiliana mtu na mkewe katika mchana wa mwezi wa Ramadhân. Vilevile, mtu anapoweka nadhiri kufunga kwa masiku mfululizo ni lazima aitekeleze nadhiri hiyo. Pia kuna sampuli fulani ya saumu ambayo haitekelezwi kwa mfululizo, kama vile kuzilipa siku za Ramadhân, kufunga siku kumi iwapo mtu hana kichinjo, saumu ya kafaarat yameen (kulingana na Jamhuri ya wanavyuoni), saumu kwa ajili ya kulipa kutokana na makosa ya hukmu za Ihraam (kulingana na rai iliyo na nguvu) na kufunga kwa ajili ya kutekeleza kiapo iwapo mtu hakunuiliya kufunga kwa masiku mfululizo.

7. Saumu za Sunnah zilizokuja kwa ajili ya kuziba pengo katika Saumu za waajib. Mifano ya saumu za waajib ni kama 'Aashooraa', 'Arafah, Ayyaamul Beedh [tarehe 13th , 14th na15th za miezi ya Hijri], Saumu za Jumatatu na Alkhamisi, siku sita za Shawwaal, na kufunga zaidi katika mwezi wa Muharram na Sha'baan.

8. Hairuhusiwi kuipwekesha siku ya ljumaa kwa kufunga. [al-Bukhaari, Fat-h al-Baari No. 1985], au kufunga siku ya ljumamosi, isipokuwa ikiwa ni Saumu ya faradhi. [Imepokewa na kuorodheshwa kuwa hasan na at-Tirmidhee 3/111] - lililomaanishwa hapa ni kuipwekesha bila ya sababu yoyote. Hairuhusiwi kufunga katika maisha yote ya mtu, au kufunga kwa siku mbili au zaidi bila ya kusimama, yaani kufunga siku mbili au tatu bila ya kusimama katikati yake. Ni *haraam* kufunga katika siku za 'Eid Mbili, au katika Ayyaam Tashreeq, ambazo ni tarehe11th,12th na13th za Dhu'l-Hijjah, kwa sababu hizi ni siku za kula na kunywa na kumkumbuka Allaah, lakini yaruhusiwa kwa mtu asiyekuwa na kichinjo kuzifunga siku hizo (Ayyaam at-Tashreeq) akiwa Mina.

قافلة الرحمة للحج والعمرة Al-Rahma `Umrah & Hajj Agencies1432

Hijri / 2011 C.E

Assalaamu `Alaykum Warahmatullaahi Wabarakaatuh:

Tunafuraha kuwajulisha yakwamba Insha Allaah Safari yetu ya mwaka huu 1432 Hijri/2011 ya kupeleka watu `Umrah katika mwezi wa Ramadhân, kumi la mwisho. Na vilevile katika `Ibaadah ya Hijjah.

Mipangilio ya Safari ya `Umrah (Mwezi wa Ramadhân) ni kama ifuatayo:

• Kuondoka ni tarehe 17 ya mwezi wa Ramadhân*Kurudi ni baada ya `Eid Insha Allaah

• Safari itaanzia Nairobi – Jeddah

• Gharama ya Safari (ikiwemo Hoteli na Usafiri) ni $1500 U.S

• Siku tatu tutakuwa Madinah na Siku kumi za mwisho tutakuwa Makkah mpaka `Eid.

• Safari ya Kurudi Jeddah – Nairobi. Itakuwa baada ya `Eid

Twapenda kuwahimiza wale wale wenye niya ya kwenda na sisi waharakishe kuleta Passport zao na picha Nne kwa ajili ya kufanya maandalizi. Sababu ni kwamba Viza zitafungwa kabla ya mweizi wa Ramadhân kuanza.Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwa njia zifuatazo:

- Tutumie e-mail katika info@qssea.net au
- Simu nambari +254 723471820 (Abu Bilaal Athman Na'man)
- Simu nambari +254 721473181 (Abu Farida Muhammad Basawad)
- Simu nambari +254 700365253 (Muhammad Abdillaah)
- Simu nambari +254 728653863 (Dr. Ashraf)